



Sustainable Agriculture Tanzania.
Tushikamane center – Kilakala – Morogoro
P.O.Box 6369, Morogoro – Tanzania
info@kilimo.org
www.kilimo.org

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania linatangaza nafasi ya kazi ya udereva. Anahitajika mtu kwa ajili ya kusaidia shughuli zote za udereva katika ofisi zetu za Morogoro mjini. Kama unavigezo na sifa kama zilivyoorodheshwa hapo unaombwa kutuma maombi kwa ajili ya nafasi hiyo.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amefaulu kidato cha Nne (IV)
- Awe na leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua miaka miwili bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na serikali
- Awe na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la pili watafikiriwa zaidi

MAJUKUMU YA KAZI YA UDEREVA

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka wafanyakazi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kupeleka vifaa na mizigo ya ofisi maeneo mbalimbali inayohitajika
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari na kufanya kazi nyingine kadri ya atakavyoelekezwa na msimazi wake

MWOMBAJI ANABIDI AWE NA: -

1. Namba ya Nida
2. Cheti cha kuzaliwa
3. Barua ya maombi ya kazi
4. Barua ya utambulisho kutoka serikali ya kijiji unachotoka
5. Nakala za vyeti
6. Leseni ya udereva

JINSI YA KUOMBA

Waombaji wote watakiwa kutuma maombi yao kwa njia ya barua moja kwa moja au kupitia barua pepe kwenda kwa hr@kilimo.org

Meneja rasilimali watu
Sustainable Agriculture Tanzania
S.L.P 6369,
Morogoro

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 10/06/2022

Kwa Mawasiliano Zaidi unaweza piga namba: 0654 329 858